




LISTEN TO "MITIKI YETU " ON RADIO PAMBAZUKO 89.5 FM EVERY FRIDAY 1930 - 2000 & SATURDAY 0730-0800

KVTC SINCE 1992

# Kutoka Dawati la Irvine

**CORONA INAUWA, OSHA MIKONO MARA KWA MARA**

Kijarida cha KVTC sasa kitakuwa kinachapishwa mara mbili kwa mwaka. Hii ni Makala ya kwanza kwa 2021.
Kokote uliko vaa barakoa na ishi salama.

## Miaka 10 KVTC kama Meneja Mkuu wa Msitu

Na Jan Leon Viljoen

Nilifika KVTC Agosti 2010 nikiwa na uzoefu wa miaka 25 ya kilimo cha misitu kibiashara na sikuwa na utaalamu wa ukuzaji mitiki. Nilipanga kukaa miaka miwili KVTC. Baada ya miaka miwiili, KVTC ilihuisha mikataba yangu, mfululizo wa kuisha mikataba ilikoma Disemba 2020. Nilijifunza haraka juu ya ukuzaji mitiki. Kama nahitajika kuelezea mambo ya muhimu katika mda wangu KVTC ni yafuatayo

Mara baada ya kuwasili KVTC niligundua mpangilio wa uvunaji unahitaji uboreshaji na katikati 2011 tulifanya muundo mwingine ambao uliongeza ujazo wa 5% kwa ha.

Mwaka 2010 KVTC ilikuwa inavuna ujazo wa 16,000 m³ na 2011 kiasi cha 22,000 m³ na 2020 KVTC inavuna kiasi cha 36,000 m³. Kuanzia 2011 – 2014 ujazo mwingi ulitoka kwenye mapunguzo. Na 2020 kiasi cha 80% kutoka kwenye mvuno wa mwisho wa shamba.


KVTC ilianzisha program kubwa kabisa ya uboreshaji wa miti ya mitiki 2013 na bado inaendelea. Moja ya mazao ya kwanza ya uboreshaji inapatikana bustanini na tunapanga kuisambaza kibiashara 2023. KVTC vilevile ilitekeleza mpango wa utafiti na maendeleo 2013 chini ya usaidizi wa Andrew Callister kama mshauri wa KVTC juu ya utafiti na maendeleo.

Kuanzia 2018 nilianza kumfundisha Geofrey Kessy aliyekuwa meneja wa ukuzaji Miti KVTC kuchukua nafasi kama Meneja Mkuu wa Misitu ifikiapo January 2021.

**Majukumu ya Mbele kwa Leon Viljoen**.

Kisicho furahisha, kustaafu mapema siyo malengo yangu sasa naenda kule nilikokuwa nafanya kabla kama mshauri wa misitu KVTC. Nitakuwa Robertson Magharibi ya Cape Winelands Afrika Kusini. Nitafanya kazi kwa mbali kama mshauri wa KVTC na nitatembelea KVTC mara 4 kwa mwaka.

## Uzoefu na KVTC (Kitengo cha Misitu)



Na: Geofrey Kessy

***a) Kujiunga na KVTC***

Ilikuwa Julai 1 2013 nilipopewa fursa kujiunga na timu ya mameneja wa misitu KVTC kama meneja wa shamba. Nilivutiwa sana kwa kuwa ilikuwa ni uzoefu wangu wa kwanza katika kilimo biashara cha misitu na kufikiria siku za nyuma nakubali kuwa yalikuwa mengi ya kujifunza kuliko nilichoweza kufanya. Ilikuwa ni upendeleo kwangu kama Mtanzania kijana mhitimu wa misitu kujifunza biashara kilimo cha misitu inayoendeshwa kwa weredi ambako kuna maeneo mengi na fursa nyingi za kujifunza na kukuza taaluma yangu.

***b) Kuimarika na timu***

Baada ya kujiunga kama Meneja wa Shamba nilipewa shamba la kusimamia shughuli za ukuzaji miti siku hadi siku. Hii ilijumuisha maandalizi ya ardhi, kupanda, kuhudumia miti iliyopandwa kutoka palilizi mpaka kupogolea matawi, ulinzi wa moto, na uzuiaji. Ilikuwa na changamoto kwa wakati huo.

Kutoka Meneja wa shamba mapema 2014, nilihamishiwa kwenye kitengo cha Mipango na utafiti kama Meneja Msaidizi nilihusika na usimamizi wa bustani, kazi ya kupanga na utafiti wakati KVTC inaendesha program kubwa ya uboreshaji wa miti. Baadhi ya kazi ninayo jivunia kwa wakati huo ni mafanikio ya kutengeneza jaribio la kwanza la vina saba katika shamba la A28 Ichima na B24 Narubungo.

Juni Mosi 2016 nilipandishwa cheo kuwa Meneja wa Ukuzaji Miti na jukumu lango lilikuwa ni kuongoza mameneja wa mashamba wa tano katika shughuli za siku hadi siku za ukuzaji miti na katika nafasi hiyo, mimi mwenyewe na timu tunajivunia hekta kadhaa kwa mafanikio ziliendelezwa katika mzunguko wa pili.

Zaidi ya kujifunza nikiwa kazini, KVTC imenipa fursa kadhaa kuhudhuria mafunzo na warsha kwa lengo la kuniimarisha kitaaluma ndani na nje ya nchi na ninashukuru kwa hilo.

***c) Kuongoza timu***

Kati kati ya 2020 nilipandishwa cheo nakuwa Meneja msaidizi wa Misitu na Januari 2021

kuwa Meneja Mkuu wa Misitu. Nafahamu hii ina majukumu yenye changamoto sana hata hivyo nimevutiwa, na moja nitajitoa kwa vyovyote kufanikisha. Kitengo cha misitu kina timu ya vijana wenye vipaji vingi kwa pamoja tutasonga mbele. Kwa sisi kama timu ni Imani uongozi wa juu umetupa sisi na hicho tunaona kama kitengo, na kwa hilo tutahakikisha tunayafikia malengo yote yaliyopangwa.

Lengo langu kwenye kitengo kwa miaka ijayo 2 hadi 3kwanza ni kuona KVTC inaanza kutumia kibiashara matokeo ya program ya mradi wa utafiti +20. Hii itajumuisha kuthibitisha na kutekeleza mfumo mzuri wa kupunguzia miti na uendelezaji wa program ya kuweka mbolea.



## Yusta Abel

**Meneja wa Misitu ya Kupandwa.**

**Wasifa Binafsi**

Yusta ni dada mwenye kipaji, hajaolewa, ana umri wa miaka 25 kutoka Dar es Salaam. Alijiunga na KVTC timu October 2020 kama Meneja wa Misitu ya kupandwa kwa mafunzo.

**Wasifa wa Kitaaluma**

Yusta kitaaluma ni Afisa Misitu aliyehitimu digrii ya sayansi ya Misitu Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Ametokea moja kwa moja kutoka chuoni na kwa miezi sita, amepata kujifunza yote katika fani ya misitu hapa KVTC.

**Uelimishaji**

Zaidi ya mafunzo ya msingi , anapata kujifunza / kuona shughuli za mashambani ikiwa Pamoja na kazi za bustani, upandaji miti, usimamizi wa maotea, uzuiaji magugu, kupunguzia matawi, kupunguzia miti, uvunaji na usafirishaji magogo kiwandani yote ya yote ni kutambua umuhimu wa afya na usalama wa wafanyakazi kazini. Bustanini amejifunza ujuzi jinsi ya kuziandaa mbegu kabla ya kupanda, ukuzaji miche, uandaaji stump na uzalishaji wa clones na uhudumiaji wa bustani kwa ujumla.

**Malengo Makuu ya Yusta KVTC**

"Kulinda uoto wa asili na binowai, kusimamia kila shamba vizuri ili kupata mavuno makubwa na kutoa mbao zenye ubora wa juu".

## Kijiji cha Mavimba kupata Mabanzi bure

Na Kennedy Haule



Agosti 19, 2020 ilikuwa siku ya kwanza kwa wananchi wa kawaida wa Mavimba kupata mabanzi bure kutoka kiwanda cha KVTC. Hadi watu 250 walijitokeza Jumatano kukusanya mabanzi.

Hussein Abdallah Manjoti (41) baba wa Watoto wanne ni mnufaikaji wa mabanzi bure kutoka KVTC. Anashukuru kupata mabanzi bure hii imesaidia kubadilisha uchumi wa kaya yake. Hussein ni fundi seremala anayetumia mabanzi kutengeneza meza, viti vya ofisini, vitanda na samani nyinginezo. Ametumia mabanzi kutengeneza kibanda kwa mtoto wake wakiume, aliyehitimu masomo ya sekondari kuanzisha biashara ya huduma za simu za mkononi. Mradi wa kutengeneza samani umekuwa nyongeza ya kipato kwa shughuli yake ya kilimo cha kujikimu. Hussein anauza samani za bei nafuu kwa watu wa kawaida hapo kijijini, hivyo kuboresha ubora wa maisha ya watu.

Mabanzi yametengeneza fursa ya kujiajiri katika sekta isiyo rasmi ya kujiajiri kwa sababu mbao kutoka miti ya asili imetoweka na kama inapatikana ni ya ghali san ana mara nyingi kutoka vyanzo visivyo halali na siyo endelevu.

Juma Ramadhani (54), ameoa na baba wa watoto watatu kutoka shinyanga amehamia mavimba hivi karibuni.

Anathibitisha kuwa bila mabanzi uhamiaji wake ungekuwa mgumu sana. Ametumia mabanzi kujenga nyumba tatu, banda la mifugo la kutunzia ng'ombe.

**Manufaa Mengine**

Mahusiano kati ya Wafanyakazi wa kampuni ya ulinzi KVTC na wananchi yameboreka kwa kiasi kikubwa. Wizi wa mbao kiwandani kwa kiasi kikubwa umetoweka.

Uamuzi wa kuruhusi wananchi kuchukua mabanzi umeboresha mtazamo chanya wa kampuni kwa wananchi wa kawaida kwa sababu ina athari za moja kwa moja katika uchumi wao wa kila siku.

## Maeneo yenye Mvuto Maalumu KVTC

*Na Joseph John*

Maeneo yenye Mvuto Maalumu KVTC (ASI) ni maeneo yenye uhitaji wa uangalizi maalumu. Haya ni maeneo yanajumuisha mvuto wa kimamazingira, mambo ya kale, historia, utamaduni na tafiti.

Mti wa Mpingo (African black wood) kwa jina la kisayansi 'Dalbergia melanoxylon' ni sehemu ya uhifadhi yenye usimamizi maalumu katika eneo la KVTC.

Aina ya mti huu nyama zake zimejizungusha , unamatawi mengi yanayokuwa taratibu sana, kufikia umri wa kuweza kuvuna kati ya miaka 70 hadi 100. Inakua katika mazingira mengi kuwa sehemu muhimu ya mfumo wa ikolojia , ikiwemo misitu ya miombo ya wazi.

KVTC inayatambua maeneo yote yenye mpingo na kuyalinda kutoka kwa majangili. KVTC inafuatilia miti hii kulingana na mahitaji ya FSC na ISO 14001. Wageni na watalii wanakaribishwa kutembelea eneo hili.

